GENDER EQUALITY IN SADC
THE TIME IS NOW

# PROTOKALI YA JINSIA NA MAENDELEO KWA NCHI ZA SADC

## IMEPITISHWA 17 AGOSTI 2008

***Protokali ya Jinsia na Maendeleo kwa nchi za SADC:***

### IMETOA DIRA

kwa ahadi zilizowekwa na nchi zote, kwa dunia na mabara yote kwa kuhakikisha usawa wa kijinsia unafanikiwa.

### IMEONGEZEA

kuwepo kwa makubaliano ya kisheria haya yameainisha mapungufu yote na kuyaziba kikamilifu, kwa kuweka malengo yenye vipimo katika maeneo yote ambayo awali hayakuhusishwa.

### ITAZIDISHA

usawa wa jinsia kwa kuhakikisha uwajibikaji kwa wajumbe wote wa nchi za SADC,pamoja na kutoa nafasi kwa jumuiya nyinginezo kuweza kutoa na kuchangia uzoefu wao katika utekelezaji wa mafanikio mazuri kijinsia, utoaji msaada na masahihisho ambayo yataleta marekebisho.









# MTAZAMO WA PROTOKALI YA JINSIA NA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA

## MAAMUZI MAKUBWA

### KIFUNGU CHA 4 - 8: KATIBA NA HAKI YA SHERIA, UPATIKANAJI WA HAKI

Kufikia mwaka 2015:

- Katiba zote katika ukanda wa kusini ni vema zihakikishe kuwa zimeweka vifungu maalumu vya usawa wa jinsia na kuhakikisha kuwa vifungu hivyo maalumu havisababishi migongano ya aina yeyote ile kisheria kwa matumizi yeyote. Na iwe hivyo hata kati ya mwanamke na mwanaume katika ndoa.
- Nchi zote ni lazima ziondokane na aina yeyote ya ubaguzi kisheria na zihakikishe zimeondoa "hali ya uchache kwa wanawake" au kisheria hali yeyote ile inayomfanya mwanamke awe tegemezi kwa upande wa baba yake, mumewe, watoto wake wa kiume au jamaa zake wowote walio wanaume.

Kufikia mwaka 2015:

✓ Katiba ya Tanzania imeridhia kuwepo kwa usawa wa jinsia, ingawa mpaka sasa bado zipo baadhi ya sheria zinazofuata mila za baadhi ya makabila ya Tanzania zinakinzana na katiba.Mpaka kufikia mwaka 2015 yapo marekebisho makubwa yatakayokuwa yamefikiwa na serikali ya Tanzania kwa kushirikisha asasi za kiraia.

✓ Nchi ya Tanzania imeshaonyesha nia ya kupambana na baadhi ya sheria kandamizi ili kuwawezesha wanawake waweze pia kurithi mali zao na siyo kuwa wategemezi kwa baba, waume, watoto wao wa kiume pamoja na ndugu yeyote wakiume.

### KIFUNGU CHA 9: WATU WENYE ULEMAVU

- Watu wenye ulemavu ni lazima wawe na afya, ustawi mwema pamoja na haki nyinginezo na ulinzi wa kutosha.

✓ Sheria ya Kazi na mahusiano ya kazi ya 2006 nambari 6, inatilia mkazo usawa katika kazi na kuondoa kwa ubaguzi. Waajiri kuhamasisha usawa na kuondoa ubaguzi, hii pia ipo katika Katiba ya nchi ya Tanzania Kipengele cha 22(2) kinasema kwamba ni haki ya kila mtu kujua, Kipengele cha 23(1)kinasema kwamba kila mfanyakazi anayo haki ya kutendewa sawa.

✓ Aidha, katika mkukuta kipengele cha III cha uongozi na uwajibikaji, walemavu wanapewa kipaumbele. Aidha, Lengo namba 4 katika Mkukuta linaelezea jinsi gani waathirika mbalimbali wakiwemo walemavu kuwa wanahitaji ulinzi na hamasa kisheria.

### KIFUNGU CHA 10: HAKI ZA WAJANE WANAWAKE NA WANAUME

- Labda iamuliwe vingine na mahakama, wajane wa kike moja kwa moja ni vema wawe chini ya uangalizi na himaya ya watoto wake, wawe na haki ya kuendelea kuishi katika makazi yake aliyoolewa na awe na gawiwo sawa la urithi kutoka kwa mumewe marehemu.
- Mjane wa kike aweze kuwa na haki ya kuolewa tena na mtu wa chaguo lake na awe na ulinzi wa kutosha na asifanyiwe fujo zozote. Haki kama hizi pia ziwepo kwa wajane wanaume wanapofiwa na wake zao.

✓ Serikali ya Tanzania bado inatumia sheria ya mirathi ya kimila ambayo mjane wa kike na watoto wa kike hawana haki ya kurithi mali ya mume/baba marehemu. Ingawa tayari shinikizo la asasi za kiraia zimetoa angalizo kwa serikali. Aidha, harakati zimeanza kufanyika kuhakikisha mwaka huu 2009 maoni ya wananchi yatakusanywa kabla ya kubadilishwa kwa sheria ya mirathi Tanzania. Waislamu wanatumia sheria ya kiislamu.

✓ Hakuna sheria inayoongelea kuhusu hatima ya mjane mwanamke au mwanume. Tamaduni mbalimbali zimeweka vikwazo kwa mjane mwanamke anayetaka kuolewa tena aweze kuhama na kumfuata mwanaume anayemuoa, na kwa mwanaume hakuna zuio lolote mpaka sasa.

### KIFUNGU CHA 11: MTOTO WA KIKE NA WAKIUME

- Sera, mipango na sheria ni lazima viwepo katika kuhakikisha vinalinda maendeleo ya watoto wote wa kiume na wakike, ikiwa ni pamoja na kuondoa aina zote za mifumo ya ubaguzi ndani ya familia, jumuiya za kijamii, taasisi na serikali.
- Desturi zozote zenye kuleta madhara pamoja na matendo mabaya dhidi ya watoto ni lazima yakomeshwe, ikiwa ni pamoja na uonevu na unyorwaji kiuchumi.
- Ni vema uwepo usawa katika masuala ya elimu na afya.

✓ Serikali ya Tanzania imeridhia mkataba wa haki ya mtoto mwaka 1989. Ingawa mpaka sasa hakuna sheria rasmi ya mtoto. Sheria ya kazi ya mwaka 2006 pamoja na Ustawi wa Mtoto katika African Charter ya mwaka 1999 kipengele cha 15 kinaelezea kuwa Tanzania imetambua umuhimu wa mtoto wa kike na kiume na tayari imekataza mtoto kutumika/kufanyishwa kazi zozote za kuajiriwa na zile za hatari na nyinginezo zozote ambazo zitaathiri mtoto kiakili. Ingawaje watanzania wengi wanaishi katika lindi la umaskini hali ambayo imeleta ugumu katika kutekeleza hilo.

✓ Sheria ya masuala ya kujamiiana ya mwaka 1998, inaelezea tohara/kukeketa mtoto wa kike ni kosa la jinai, ingawa jamii nyingi bado inaendeleza.

✓ Serikali ya Tanzania pamoja na sera ya elimu na afya imeweka kipaumbele kwa watoto wote, ila mpaka sasa utekelezaji wake ni mgumu kutokana elimu ndogo kwa jamii pamoja na umasikini uliokithiri jamii nyingi hutoa kipaumbele kwa kumpa elimu mtoto wa kiume pekee. Kumekuwa na shule nyingi za msingi ambazo zinakosa vyoo imara na maji mazingira ambayo mtoto wa kike hataweza kumudu. Vilevile tatizo la mimba katika umri mdogo limekuwa kubwa kwa watoto wa shule za msingi. Hatua iliyochukuliwa na serikali katika kukabiliana na hali hiyo ni pamoja na kushirikisha jamii katia ujenzi wa shule za msingi na sekondari katika kila kata.

### KIFUNGU CHA 12-13: UTAWALA (UWAKILISHI NA USHIRIKISHWAJI)

- Kufikia mwaka 2015 wanawake ni vema wakashika angalau nusu ya nafasi zile zenye maamuzi katika SADC, sekta binafsi na serikali (Ikiwa ni pamoja na bungeni, serikali za mitaa na nafasi za uwaziri.)
- Nchi wanachama ni lazima wahakikishe kuwa wanawake wanashiriki kikamilifu katika chaguzi mbalimbali pamoja na kutoa maamuzi kwa kujengewa uwezo, wanawake wawezeshwe ili wawe na nguvu ya kuhamasisha maamuzi yenye sura ya kijinsia.

✓ Kufikia mwaka 2015, serikali ya Tanzania imefanya mikakati ambayo itaweza kufikia malengo ya 50/50. Mpaka sasa katika wiliaya 120, robo ya wakuu wa wilaya ni wanawake, aidha wapo wanawake ambao ni wakuu wa mikoa, makatibu wakuu wa wizara, manaibu waziri na mawaziri pamoja na wabunge wanawake ambao mpaka sasa ni 30%, aidha, vilevile kwenye sekta binafsi wanawake wanapata nafasi na wanaume.

✓ Katika utekelezaji wake serikali ya Tanzania imeridhia mkataba wa CEDAW, tayari ipo wizara ya Jinsia, Maendeleo ya jamii na Watoto ambayo hushughulika na masuala ya Jinsia kwa undani wake ikiwemo kuwajengea uwezo na kuhamasisha wanawake kugombea nafasi mbalimbali kwa kutoa elimu ya jinsia kwa jamii wakishirikiana na asasi mbalimbali za kijamii.

### KIFUNGU CHA 14: ELIMU NA MAFUNZO

Kufikia mwaka 2015:

- Kutakuwepo na usawa na haki ya elimu na mafunzo kwa wanawake na wanaume katika viwango mbalimbali vya elimu.
- Kutakuwepo na sera ya elimu ya jinsia na mipango yenye madhumuni yenye kutoa changamoto katika kuondoa ukandamizwaji na kuondoa kabisa uonevu wa kijinsia katika taasisi zote za elimu.

Kufikia mwaka 2015:

✓ Sera ya elimu Tanzania kuanzia elimu ya chini mpaka ya juu imezingatia elimu sawa kwa wote, ambapo imetoa kipaumbele kwa wanawake kama vile kuhakikisha wanawake wanapata nafasi ya kutosha katika masomo ya sayansi. Sasa hivi kuna mikopo ya fedha ya elimu ya juu ambapo wanawake wanayo nafasi kubwa ya kuomba na kupata mikopo kwa ajili ya kujisomesha.

✓ Sera ya elimu ya juu nchini, somo la jinsia ni la muhimu (Core subject) ambapo mwaka wa kwanza na wapili husoma. Katika elimu ya msingi somo la Uraia linamafundisho ya jinsia. Kwa ufupi Jinsia imepewa kipaumbele katika elimu ya Tanzania. Tunaimani kuwa ifikapo mwaka 2015 mikakati mingi zaidi katika kuhakikisha jinsia inapewa kipaumbele itakuwa imekamilika.

### KIFUNGU CHA 15-19: RASLIMALI ZALISHI NA AJIRA, NGUVU YA UCHUMI

Kufikia mwaka 2015, serikali inatakiwa

- Kuhakikisha kuwa ushirikishwaji sawa wa wanawake na wanaume kwenye unanzishwaji wa sera za uchumi na uendelezwaji wake.
- Utoaji/ugawaji sawa wa maliasili kwa kuzingatia jinsia na matakwa sawa kati ya wanawake na wanaume.
- Kuhakikisha usawa kwa wote, faida na nafasi kwa wanawake na wanaume kwa ajili ya kufanya biashara na ujasiriamali, pamoja na njia zote za upataji wa zabuni mbalimbali.
- Kupitia upya sera na sheria zinazowezesha mwanamke kumwongezea tija katika uzalishaji wa mali, vitu ambavyo vitawaongezea tija wanawake ni kama vile

Kufikia mwaka 2015, serikali inatakiwa kuwa:

✓ Sera ya serikali katika kuhakikisha wanawake na wanaume wanakuwa sawa kiuchumi, lakini bado kuna vikwazo vinavyosababisha wanawake kushindwa kama vile kuwa na hati za nyumba au shamba ili waweze kupata mkopo. Kufikia mwaka 2015 zipo dalili za kufanikiwa.

✓ Bajeti ya kila mwaka bado haijazingatia mahitaji ya jinsia hasa kwa upande wa wanawake mfano mahitaji muhimu kama vile maji, nishati, vifaa vya uzazi pamoja na vya kujihifadhia wanawake. Ifikapo mwaka 2015 mafanikio kidogo yatakuwepo hasa baada ya asasi za kiraia kutilia mkazo suala hilo.

✓ Serikali inaweza ikawa imekidhi haja ya jinsia zote katika kutoa nafasi ya ujasiriamali pamoja na masuala ya zabuni ifikapo 2015 ila elimu ya uwiano huo bado inahitajika.

✓ Mpaka sasa sheria mpya za ardhi (na.4 na.5) za mwaka 1999 na sheria ya Mahakama zinazoshughulikia migogoro ya ardhi 2002 kipengele cha 114 zinatambua haki ya kila mwanamke kuhodhi na kutumia ardhi sawa na mwanaume. Kuhusu suala la Maji, mwezi Disemba.

## MAAMUZI MAKUBWA

ardhi na maji.
- Kuhakikisha wanawake na wanaume wanakuwa na usawa kiuchumi katika kazi za kuajiriwa katika kila idara.

mwaka 2006 serikali ilipitia na kurekebisha upya sera ya maji na idara zake na ilipitishwa na bunge mwaka 2007. Sera ya ardhi na ya maji, mpaka sasa bado serikali haijaweza kumsaidia mwanamke ambaye ndiye mtumiaji mkubwa wa ardhi na maji, elimu zaidi inahitajika kwa ushirikiano na asasi zisizo za kiserikali kuhakikisha mwaka 2015 jamii iwe imejikwamua.
- ✓ Sheria ya kazi ya Tanzania inapigania haki sawa ya ajira kwa wanawake na wanaume, utekelezaji mpaka sasa bado haujapewa kipaumbele, kutokana na hamasa mbalimbali zinazofanywa na asasi mbalimbali mpaka 2015 upo uwezekano kwa asilimia 70 kufanikiwa.

### KIFUNGU CHA 20-25: UONEVU WA KIJINSIA

Kufikia mwaka 2015 serikali za nchi zitakuwa:-
- Zimehakikisha sheria zilizopitishwa au kuanzishwa zinazuia kila aina ya unyanyasaji wa kijinsia na kuhakikisha wakosaji wote wanachukuliwa hatua kisheria.
- Hatua zichukuliwe katika kukatisha tamaa muendelezo wa mila potofu na vitendo ambavyo vinachangia matatizo na unyanyasaji wa kijinsia.
- Kuhakikisha kuwa sheria za unyanyasaji wa kijinsia zinakuwepo na zinakidhi haja zote muhimu kama vile kwa kutoa matibabu na matunzo kwa waathirika.
- Kuhakikisha kuwa kunakuwepo mbinu mbadala kwa waathirika kupatiwa ushauri nasaha kwa wote wenye matatizo ya kuathiriwa au kuathirika kijinsia.
- Zitungwe sheria zinazozuia matendo ya biashara ya kuuza na kusafirisha watu na kutoa ushauri na huduma kwa walioathirika kwa hilo.
- Zitungwe sheria, sera na mipango ya kuondoa kabisa manyanyaso ya kijinsia.
- Kuwepo na misaada pamoja na huduma ya kutosha, taarifa, mafunzo ya jinsia na elimu kwa watoa huduma wote wa aina mbalimbali.
- Kufanikiwa kupunguza matatizo ya unyanyasaji kijinsia kwa kiwango cha nusu kutoka katika hali ya sasa.

Kufikia mwaka 2015 serikali itakuwa:
- ✓ Imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wake katika kuzuia aina zote za mifumo mbalimbali isiyozingatia jinsia, kwani mpaka sasa tayari kila idara ya serikali kuna kitengo kinachoshughulikia masuala ya jinsia mfano polisi na wizara zote za serikali.
- ✓ Imechukua hatua mbalimbali za kukomesha vitendo vyovyote vinavyochangia muendelezo wa unyanyasaji wa jinsia kwa aina yeyote ile, hii inadhihirisha kutokana na kutilia mkazo masuala ya jinsia kwa viwango tofauti kwa kutoa elimu kwa kushirikiana na asasi za kiraia na vyombo vya habari.
- ✓ Hatua zaidi zitajengeka ifikapo mwaka 2015, kwani hata sasa hivi kupitia katika sheria ya masuala ya kujamiiana ya mwaka 1998 (SOSPA) tayari inahakikisha kuwa waathirika wanapata matibabu na uangalizi baada ya tatizo kutolewa taarifa katika vituo vya polisi na sheria kufuatwa.
- ✓ Vituo vya ushauri nasaha vya serikali na mashirika mbalimbali vitaongezeka zaidi na kuhamasiha waathirika kujitokeza kwa wingi ili kupatiwa huduma hiyo muhimu. Hii inachangiwa na hamasa inayofanywa kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini.
- ✓ Kwa kuwa sheria ya masuala ya kujamiiana ipo,na tayari inazungumzia makosa ya kusafirisha/kupelekwa kufanya kazi mbalimbali hasa kwa watoto wa kike ifikapo mwaka 2015 wananchi wengi na hasa wa vijijini watakuwa wamehamasishwa zaidi na kuacha kushiriki katika vitendo vya usafirishaji wa watu hasa watoto wakike kwa ajili ya kwenda kupatiwa ajira kinyume na sheria za nchi, badala yake watoto wengi wa kike watabaki mashuleni.
- ✓ Sheria ya masuala ya kujamiiana ipo, ifikapo mwaka 2015 vipengele ambavyo vinaleta utata vitakuwa vimeshatatuliwa na jitihada hizo zimeshaanza kwa ushirikiano kati ya asasi za kiraia na Wizara ya Sheria na Katiba.
- ✓ Idara na sekta nyingi za umma zitakuwa zimeshapata mwamko wa masuala ya jinsia kwa kuwa mpaka sasa elimu juu ya jinsia imeshaendelezwa kutolewa karibu kila eneo kuanzia mashuleni kwa njia ya vyombo vya habari, mafunzo kwa jamii nk.
- ✓ Tunaamini kuwa ifikapo mwaka 2015 wananchi wengi watakuwa wameshaelimika na unyanyasaji wa kijinsia utapungua kwa kiasi kikubwa.

### KIFUNGU CHA 26: AFYA

- Ondoa vifo vya wakina mama wazazi kwa asilimia 75%.

- ✓ Kutokana na mikakati mbalimbali inayofanywa na serikali kwa kushirikiana na asasi za kiraia tunaamini angalau kwa asilia 50 Tanzania itaweza kupunguza vifo vya watoto na wazazi.

### KIFUNGU CHA 27: VVU NA UKIMWI

Kufikia mwaka 2015, Serikali za nchi husika zinategemewa kuwa:
- Zimeendeleza mikakati ambayo ni ya kijinsia ili kuzuia maambukizi mapya.
- Zihakikishe jamii inakuwa na uwezo wa kupata matibabu ya VVU na UKIMWI kwa waathirika, wanawake, wanaume na watoto.
- Kuwepo kwa mipango thabiti ambayo itatambua kazi za watoa huduma na kuwapatia vifaa na misaada yenye ustawi.
- Wanaume waweze kushawishiwa ili watoe ushirikiano katika utoaji huduma kwa waathirika.

Ifikapo mwaka 2015, serikali inatarajia kuwa:
- ✓ Itakuwa imeandaa mikakati yenye muonekano wa kijinsia katika kuzuia maambukizi mapya, juhudi tayari zinaonekana kwa sasa.
- ✓ Kutokana na juhudi zinazoendelea kufanyika na taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali kuhakikisha kuwa waathirika wa UKIMWI wanapatiwa matibabu ya uhakika iliyoanza sasa kuweza kuendelea zaidi ili huduma iweze kupatikana kwa wingi zaidi.
- ✓ Kwa kuwa tayari serikali imeshaanzisha utekelezaji wa masuala mbalimbali kwa kutoa huduma kwa waathirika wa UKIMWI, ifikapo mwaka 2015 huduma zaidi itatolewa kwa maana hata kiwango cha uchumi tunatumai kuwa kitakuwa kimeongezeka.
- ✓ Kutokana na hali ya UKIMWI kuongezeka zaidi, aidha ni hakika kuwa wanaume watahamasika zaidi katika kutoa huduma.

### KIFUNGU CHA 28: UJENZI WA AMANI PAMOJA NA USULUHISHI WA MIGOGORO

Kufikia mwaka 2015, mipango thabiti ni muhimu iwe imetekelezwa kuhakikisha kuwa upo usawa katika uwakilishi wa wanawake katika kamati za usuluhishi wa migogoro na kujenga amani hayo yote kwa kuzingatia jinsia inapewa kipaumbele si kwa taifa tu na kwa bara zima pia.

Kutokana na migogoro mbalimbali ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima kuendelea na kuleta madhara mengi zaidi, na migogoro inayotokea wakati wa uchaguzi mkuu wa serikali, mpaka ifikapo mwaka 2015 serikali ya Tanzania itakuwa tayari imeweka mkakati wa kukabiliana na hali hiyo.

### KIFUNGU CHA 29 - 31: HABARI, TAARIFA NA MAWASILIANO

Kufikia mwaka 2015:
- Jinsia ni muhimu iweze kuonekana sehemu zote za mawasiliano, taarifa na vyombo vya habari katika sera na sheria pia.
- Wanawake wawe na uwakilishi ulio sawa katika kila eneo na viwango vyote vya kazi za kihabari.
- Wanawake na wanaume ni vema wawe na sauti sawa katika kazi za habari.
- Mipango mbalimbali ipangwayo kwa ajili ya ukandamizwaji au kudhalilisha wanawake iweze kupatiwa changamoto madhubuti ili isiendelezwe.

Ifikapo mwaka 2015:
- ✓ Masuala ya jinsia katika vyombo vya habari yatakuwa yameshika kasi nzuri kutokana na mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa waandishi wa habari, aidha sera za jinsia zitaendelea kuwepo na kuhamasisha waandishi katika kutetea masuala ya jinsia.
- ✓ Kwa sasa tayari wanawake wanahabari wako katika idara nyingi muhimu katika vyombo vya habari, ifikapo mwaka 2015 wanawake watakuwa juu zaidi.
- ✓ Sera za habari na jinsia zitaimarika kuona kuwa wanawake na wanaume wanapatiwa haki sawa katika vyombo vya habari.
- ✓ Kutokana na sera ya habari na jinsia kuanzishwa katika vyombo vya habari ni wazi kuwa vipindi maalumu vya wanawake vitaendelezwa na masuala ya jinsia yatakuwa yamejidhihirisha na kuchukua sura mpya kwa vyombo vya habari.

### KIFUNGU CHA 32 - 35: UTEKELEZWAJI, USIMAMIAJI NA TATHMINI

- Utekelezwaji wa protokali uwe na usimamizi na kamati iliyoundwa kwa kuzingatia jinsia/Idara ya mawaziri wanawake, kamati ya maafisa wa juu wanaoshughulikia jinsia/ Masuala ya wanawake, na sekretarieti ya SADC.
- Kuwepo na mpango kazi mkakati wa maendeleo wa taifa kulingana na protokali ya jinsia.
- Kuwepo na ukusanyaji wa taarifa zote muhimu kwa ajili ya kuzisimamia na kuziainisha.
- Protokali hii inahitaji Nchi Wajumbe/Wanachama kuwasilisha taarifa madhubuti kwa sekretarieti kila baada ya miaka miwili na taarifa ionyeshe maendeleo na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji uliofanyika.

- ✓ Uendelezwaji wa sera ya jinsia kwa nchi za SADC katika serikali ya Tanzania utakuwa unasimamiwa na Wizara ya Jinsia, Maendeleo ya Jamii na Watoto ndiyo kazi kubwa ya wizara hiyo.
- ✓ Tayari wizara imeshapanga mikakati ya kitaifa kutokana na sera iliyopo.
- ✓ Ukusanywaji wa viashiria mbalimbali kwa ajili ya ufuatiliaji na uchambuzi wa data katika masuala ya jinsia.
- ✓ Taasisi za kiserikali kwa kushirikiana na asasi za kiraia zitakuwa zinaandaa utekelezaji wa masuala ya kijinsia.

## Uwepo wa Protokali ya Jinsia

Azimio la kuwepo kwa Protokali ya Jinsia na Maendeleo kwa nchi za SADC imekuwa ni chachu ya maendeleo na jinsia kwa nchi nyingi za ukanda wa kusini. Ikiwa na vigezo vipatavyo 30 vya kufikia malengo yaliyoainishwa ili kuweza kuwa na usawa wa kijinsia ifikapo mwaka 2015, hatua hii ya mafanikio ni ya kwanza katika dunia na imeiweka jumuiya ya SADC katika mhimili wa juu katika utambuzi wa mikakati katika kushawishi utandawazi katika bara zima la Afrika na dunia kwa kuonyesha jitihada kwa upande wa kusini mwa Afrika.



## Asasi za Kiraia ambazo zimeshiriki kikamilifu katika uanzishwaji wa Protokali ya Jinsia kwa nchi za SADC

Muungano wa Nchi za Kusini katika uanzishwaji wa Protokali ya Jinsia (Muungano)[1], kwa pamoja mataifa karibia 40 pamoja na Asasi za Kiraia zinazowakilisha kanda ya kusini zimekuwa zikiendesha kampeni toka mwaka 2005 kwa ajili kushawishi kuwepo kwa Protokali ya Jinsia na Maendeleo, kukubaliwa na nchi husika na utekelezwaji wake kufanyika kwa nchi za SADC.

Muungano huu unafanya kazi kwa makini na kwa umoja, na kuongozwa na wajumbe ambao kati yao wako katika kamati ongozi. Kamati ongozi imeundwa na mashirika yafuatayo:

- Gender Links – Mratibu kiongozi wa asasi zisizo za kiserikali (NGO); aidha ni asasi ongozi katika jumuiya zinazohusika na masuala ya Ukatili wa Kijinsia.
- Zimbabwe Women Resource Centre and Network – Asasi ongozi katika Jumuiya za Jinsia na Uchumi.
- Gender Advocacy Programme - Asasi ongozi ya Jumuiya za Jinsia na Utawala.
- Gender and Media Network of Southern Africa – Asasi ongozi ya Jumuiya ya Jinsia na Habari.
- SAfAIDS – Asasi ongozi ya Jumuiya ya Afya, mahusiano kwa njia ya kujamiiana na Haki za Uzazi, VVU na ukimwi.
- WLSA – Asasi ongozi ya Jumuiya za Katiba na Haki Sheria.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na: Asasi ya Jinsia na Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (GEMSAT), S.L.P 78172, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255 22 2129757; Faksi: +255 22 2137548; Barua Pepe: gemsa.tanzania@gmail.com; Tovuti: www.gemsa.org.za
Kwa taarifa zaidi wasiliana na: alliance@genderlinks.org.za, www.genderlinks.org.za , telefone 00 27(0)11 622 2877

1 The SADC Gender Protocol Alliance comprises: Association of Local Government (ALAN); African Women's Economic Policy Network (AWEPON); Botswana Council of NGOs (BOCONGO); Christian Council of Mozambique; CIVICUS; Federation of African Media Women (FAMW) – SA; GAP; Gender Links (GL); Gender and Media Southern Africa Network (GEMSA); Gender Policy Program Committee (Botswana); Justice and Peace (Lesotho); Malawi Council of Churches; Media Institute of Southern Africa (MISA); NGO Gender Coordination Network Malawi; SAFAIDS; SAMDI; SALGA; Society for Women and AIDS in Africa Zambia (SWAAZ); Trade Collective; Women in Law and Development in Africa (WILDAF); Women in Law in Southern Africa (WLSA); Women, Land and Water Rights Southern Africa (WLWRSA); Namibia Non-Governmental Forum (NANGOF); Women's Net; Young Women's Christian Association Botswana (YWCA); Zimbabwe Women Lawyers Association; Zimbabwe Women's Resource Centre (ZWRCN). Associate Members: African Women and Child Feature Service; Swedish Cooperative Centre - Southern Africa; Diakonia (Zambia).



2195 GEMINI CONCEPTS: ✆ 083-306-3229